# UJIRANI Mwema

HIFADHI NA JAMII

Oktoba-Desemba 2021




**MRADI REGROW KUGHARAMIA MASOMO YA VIJANA 476** UKURASA 5

**RHOBI: NYOTA ANAYETUMIA SANAA YA UIMBAJI KUHAMASISHA UHIFADHI SERENGETI** UKURASA 17

**Bodi ya Uhariri**

Mhariri Mkuu:
William Mwakilema

..............

Mhariri Mwandamizi:
Godwell Meingataki

................


Wahariri Wasaidizi:
Catherine Mbena
Samwel Nassari

...................

Mhariri Mshauri:
Claud Gwandu

...................

Wasanifu wa Kurasa:
Kitengo cha Uchapishaji - TANAPA




UJIRANI MWEMA ni jarida linalotolewa na Hifadhi za Taifa Tanzania Kitengo cha Uhifadhi Mahusiano ya Jamii, TANAPA Makao Makuu, Barabara ya Dodoma, S.L.P. 3134, Postikodi 23106 Arusha-Tanzania
Uchapishaji na kitengo cha uchapishaji TANAPA
Email: conservation@tanzaniaparks.go.tz

# YALIYOMO

3
TAHARIRI

5
MRADI WA REGROW KUGHARAMIA MASOMO YA VIJANA 476

8
HIFADHI YA MAHALE YAINUA KIPATO CHA WANANCHI

10
MAPOROMOKO YA KATERELA KIVUTIO CHA UTALII BIHARAMULO

13
UJIRANI MWEMA WACHOCHEA UHIFADHI NA MAENDELEO ENDELEVU QATESH

15
UFUGAJI NA KILIMO CHA KUHAMAHAMA TISHIO LA UHIFADHI MAHALE-KATAVI

17
RHOBI ATUMIA SANAA YA UIMBAJI KUHAMASISHA UHIFADHI SERENGETI

19
RUMANYIKA-KARAGWE YAWAFUNDA MGAMBO UHIFADHI KUCHOCHEA ULINZI WA MALIASILI

21
KISA CHA BABA NA MAMA KENGE: MFANO WA SULUHISHO LA MIGOGORO KATI YA JAMII NA HIFADHI

23
SAANANE YATUMIA MICHEZO KUHAMASISHA ELIMU YA UHIFADHI

27
MATUNDA YA ULINZI SHIRIKISHI YAANZA KUONEKANA RUAHA

30
TANAPA KUWATUMIA WALIMU NA WAELIMISHA JAMII KUTOA ELIMU YA UHIFADHI

32
HIFADHI YA ARUSHA YABORESHA MAZINGIRA YA KUJIFUNZIA NGONGONGARE

34
MKOMAZI YAWA MKOMBOZI KWA WAKAZI WA KIJIJI CHA MHEZA



# TAHARIRI



**Msomaji mpendwa**

Tunayo furaha kukualika katika Jarida letu upate nafasi ya kusoma na kupitia taarifa na habari motomoto zinazohusu masuala ya ujirani mwema kutoka katika Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA).

Jarida letu la Ujirani Mwema linaandaliwa na Kitengo cha Uhifadhi - Mahusiano ya Jamii cha TANAPA, na litatoka kila baada ya miezi mitatu.

Kupitia jarida hili, utapata fursa ya kujionea kazi mbalimbali zilizotekelezwa na maofisa wa TANAPA katika kutoa elimu ya uhifadhi kwa jamii zinazozunguka Hifadhi za Taifa, kuboresha mahusiano na jamii hizo, mafanikio yanayotokana na mchango wa TANAPA kwa jamii kupitia miradi ya ujirani mwema na ile ya kuinua kipato.

Mathalani, pamoja na kazi hizo, tunapenda kukujulisha mpendwa msomaji wetu, TANAPA kupitia mradi wa kuboresha usimamizi wa Maliasili na kukuza Utalii kusini mwa Tanzania (REGROW) unaotekelezwa katika Hifadhi ya Taifa Nyerere, Ruaha, Mikumi na Milima ya Udzungwa pamoja na maeneo mengine yenye vivutio vya utalii kusini mwa Tanzania, unatoa ufadhili wa masomo kwa vijana 476 kutoka vijiji 61 vilivyo jirani na Hifadhi hizo. Hii ni fursa kubwa sana ambayo jamii inapaswa kuitumia ili kuongeza maarifa na kuchangamkia fursa za utalii zilizopo ili jamii ipate manufaa zaidi kwa uwepo wa vivutio hivi.

TANAPA inajivunia kushirikiana na wanajamii kutoa elimu ya uhifadhi katika baadhi ya vijiji vinavyozunguka Hifadhi za Taifa. Jumla ya Hifadhi 12 zinatekeleza program hii maalum. Kwa upande mmoja, program hii inawajumuisha walimu wa masomo ya Maarifa ya Jamii darasa la tano kwa shule za msingi na somo la Jiografia kwa kidato cha pili kwa shule za sekondari kutoka vijiji jirani na Hifadhi za Taifa 10, huku ikiwatumia walelimishaji jamii kutoa elimu kwa jamii katika vijiji jirani na Hifadhi za Taifa mbili. Maendeleo mazuri ya program hii yatatoa wigo wa kuyafikia maeneo mengine zaidi ili jamii ipate uelewa wa uhifadhi.

Aidha, mpendwa msomaji, TANAPA inakualika kuzitembelea Hifadhi za Taifa ili kujionea vivutio mbalimbali ambavyo mwenyenzi Mungu ametujalia katika nchi yetu ikiwa ni pamoja na kujivunia kuwa nazo.

Ni mategemeo yetu kuwa wasomaji wa jarida hili watafurahia na kujifunza mengi. Tutafurahi kupokea maoni, ushauri na mapendekezo ili kuboresha jarida hili.

“Uhifadhi endelevu, kwa maendeleo”

“Tumerithishwa, tuwarithishe”

**Karibuni Sana.**

..................................

William Simon Mwakilema

# Ujumbe kutoka kwa mhariri



Tunayo furaha kukualika katika Jarida letu upate nafasi ya kusoma na kupitia taarifa na habari motomoto zinazohusu masuala ya ujirani mwema kutoka katika Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA).

Jarida letu la Ujirani Mwema linaandaliwa na Kitengo cha Mahusiano ya Jamii cha TANAPA, na litatoka kila baada ya miezi mitatu.

Jarida hili litaendelea kutoa fursa kwa wahifadhi na wadau wetu kupata habari zinazotoka uwandani kuhusiana na jitihada za TANAPA katika kutekeleza shughuli za uhifadhi kwa kuwashirikisha wananchi na wadau wengine pamoja na kuonyesha kwa vitendo mchango na faida ya uhifadhi kwa jamii na Taifa.

Kupitia makala mbalimbali, jarida letu litabainisha jinsi TANAPA inavyotumia mbinu na mikakati mbalimbali kujenga mahusiano na jamii, kuwashirikisha wananchi katika shughuli za uhifadhi, kutoa Elimu ya Uhifadhi, kuandaa mipango endelevu ya matumizi bora ya Ardhi, kutekeleza miradi ya kijamii na miradi ya kuongeza kipato kwa wananchi kupitia vikundi vya kijamii hivyo kuleta manufaa kwa mtu mmoja mmoja

Toleo hili lina makala mbalimbali ambazo zinaonyesha jitihada za kujenga na kuimarisha ujirani mwema kwa ushirikiano na jamii zinazoishi karibu na hifadhi. Kwa ujumla, TANAPA ina hazina kubwa na uzoefu katika kushirikisha jamii, hivyo kupitia makala mbalimbali katika jarida hili tutaendelea kuelezea na kuonyesha yale ambayo Shirika linafanya katika kuendeleza uhifadhi na kuchangia katika maendeleo ya jamii.

Ni mategemeo yetu kuwa wasomaji wa jarida hili watafurahia na kujifunza mengi. Pia, tutafurahi kupokea maoni, ushauri na mapendekezo ili kuboresha jarida hili.

**“Uhifadhi endelevu, kwa maendeleo”**

# MRADI WA REGROW KUGHARAMIA MASOMO YA VIJANA 476



Zoezi la ujazaji dodoso kutathmini uhitaji wa vijana kupata ufadhili wa masomo kupitia mradi wa REGROW likiendelea katika kijiji cha Mikumi

*David Kadomo na Innocent Epimack*

**david.kadomo@tanzaniaparks.go.tz na innocent.epimack@tanzaniaparks.go.tz**

MRADI wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW) umepanga kutoa ufadhili wa masomo kwa vijana 476 kutoka vijiji 61 vilivyo jirani na Hifadhi nne za Taifa zinazotekeleza mradi huo.

Mradi huo wenye thamani ya shilingi 345 Bilioni unatekelezwa katika Hifadhi za Taifa za Nyerere, Ruaha, Mikumi na Milima ya Udzungwa pamoja na maeneo mengine yenye vivutio vya utalii kusini mwa Tanzania.

Kwa mujibu wa sehemu ya mpango mkakati wa mradi huo, program ya ufadhili wa masomo kwa vijana hao inajumuisha vijana wa kiume 280 na vijana wa kike 196. Program hiyo itakuwa na aina mbili za ufadhili. Kwanza, itahusisha mafunzo ya muda mfupi ambayo yatafanyika kwa kipindi cha kuanzia mwezi mmoja hadi miezi sita yakihusisha nyanja za ufundi, utalii na kozi zingine zinazotoa mchango katika mnyororo wa biashara ya utalii.

Kwa upande wa mafunzo ya muda mrefu ambayo yatafanyika kuanzia mwaka mmoja na kuendelea, ufadhili utahusisha masomo

yanayohusu usimamizi wa wanyamapori, utalii na masoko, maendeleo ya jamii, upangaji na usimamizi wa miradi, ushirika na kozi zingine muhimu zitakazosaidia kufikia malengo ya mradi.

Mpango mkakati huo unaeleza kuwa, vijana hao watalipiwa gharama zote za masomo katika vyuo vya mafunzo ya kati hadi vile vya elimu ya juu ikiwa ni pamoja na vyuo vikuu ili kusaidia kupata vijana wenye ujuzi watakao shiriki kukuza utalii na uhifadhi katika maeneo yao.

"Hii itasaidia upatikanaji wa rasilimali watu wenye ujuzi na taaluma ambao watasaidia kuboresha shughuli za kiuchumi na kijamii katika vijiji nufaika," inasema sehemu ya mpango mkakati huo, na kuongeza;

"Lengo la mradi huu ni kuhakikisha shughuli za utalii zitakapoimarika kutokana na uboreshaji wa miundombinu, vijana wanaoishi jirani na Hifadhi zinazotekeleza mradi watanufaika na uwepo wa rasilimali hizo. Ukuaji wa Utalii utahitaji watu wenye ujuzi wa aina mbalimbali kuweza kuwahudumia watalii na mahitaji yao".

Katika utekelezaji wa mradi huo, baadhi ya hifadhi zilizo katika mradi, zimeanza kutekeleza mipango mbalimbali inayoshirikisha jamii zinazozunguka hifadhi hizo kwa mafanikio.

**Hifadhi ya Taifa ya Nyerere**

Ikiwa ni miongoni mwa hifadhi zinazotekeleza mradi wa REGROW, Hifadhi ya Taifa Nyerere inatekeleza miradi yenye thamani ya sh 85.1 bilioni inayohusisha ujenzi wa viwanja vya ndege katika maeneo ya Matambwe, Mtemere, Kibambawe, Kinyanguru, Nzasa na Mtende.

Aidha, mradi huu utaimarisha miundombinu ya barabara ndani ya hifadhi, kununua vifaa vya doria na vitendeakazi vingine vya hifadhi.

Katika hifadhi hiyo, mradi pia utatoa mafunzo kwa vikundi vya wajasiriamali kutoka katika vijiji jirani ikiwa ni pamoja na kuwatafutia masoko ya bidhaa zao na kuwapa elimu ya uhifadhi na mazingira.

Vikundi hivyo ambavyo vinalenga kuinua na kukuza pato la wananchi, vipo katika vijiji vya Magogoni, Dakawa, Kisaki Kituoni, Nyange na Msolwa Stesheni.

Baadhi ya wanufaika wa mradi huo wameahidi kulinda maliasili kama wanavyolinda wazazi wao kutokana



Zoezi la ujazaji dodoso kutathmini uhitaji wa vijana kupata ufadhili wa masomo kupitia mradi wa REGROW likiendelea katika kijiji cha Mikumi



Mhifadhi ujirani mwema David Kadomo kutoka Mikumi akitoa maelezo katika kikao

na manufaa wanayotegemea kutoka kwenye mradi.

“Tutailinda hifadhi ya Nyerere na vilivyomo kama wazazi wetu, hatutakubali mtu au kikundi cha watu wavuruge maliasili zilizomo, maana tunafaidika nazo, maisha yetu yatasonga mbele kutokana na wageni watakaoingia kuona wanyama” alisema Jamila Bomeza, Mwezeshaji jamii kutoka kijiji cha Kisaki Kituoni.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Magogoni, Athumani Zingizi alisema “kutokana na ushirikishwaji wa kijiji chetu kwenye mradi, nitahakikisha katika kila mkutano wa hadhara, nazungumzia kwa uzito ajenda ya utalii wa ndani na ulinzi shirikishi wa maliasili”.

**Hifadhi ya Taifa Mikumi**

Chini ya mradi wa REGROW, vijiji nane vilivyopo jirani na Hifadhi vitanufaika na mradi huo. Vijiji hivyo ni Mikumi, Ihombwe, Kilangali na Tindiga vilivyopo wilayani Kilosa, na vijiji vya Mkata, Doma, Maharaka na Sewe-Kitera vilivyopo wilayani Mvomero Mkoa wa Morogoro.

**Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa**

Kwa upande wa Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa, vijiji 13 vitanufaika na mradi. Vijiji hivyo ni Mkamba, Kidatu, Mang’ula B, Msufini, Kanolo, Mkula, Msolwa ujamaa na Kiberege wilayani Kilombero, mkoani Morogoro pamoja na vijiji vya Msosa, Ikula, Wotalisoli na Udekwa vilivyopo wilaya ya Kilolo mkoani Iringa.

**Hifadhi ya Taifa Ruaha**

Vijiji 16 vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa Ruaha vitanufaika na mradi wa REGROW. Vijiji hivyo ni Makuka, Mboliboli, Kinyika, Itunundu, Kisanga, Malinzanga, Mahuninga, Idodi, Tungamalenga, Isele, Mafuruto na Makifu vilivyopo wilayani Iringa Mkoa wa Iringa. Vijiji vingine ni Mapogoro kilichopo wilayani Mbarali Mkoa wa Mbeya na Ilangali, Manda na Chinugulu vilivyopo wilayani Chamwino Mkoa wa Dodoma.



# HIFADHI YA MAHALE YAINUA KIPATO CHA WANANCHI



Wanakikundi wakiwa katika shughuli za kila siku (mashine ya kuvnja mise)

**Na Fredrick Mhalafu**

**fredrick.mhalafu@tanzaniaparks.go.tz**

“Tunaishukuru sana TANAPA kupitia Hifadhi ya Mahale kwa kutuwezesha mradi huu wa kukamua mafuta ya mawese, kuvunja ngazi na kukamua mafuta ya mise... hakika huu ni ukombozi”, alisema Gwahula Mahamoud, mkazi wa Kijiji cha Kalya.

Mahamoud ni mmoja wa wanachama 29 wa kikundi cha Kijamii cha Uhifadhi wa Kuweka na Kukopa (COCOBA) cha Lubugwe kilichopo katika kijiji cha Kalya, kata ya Kalya wilaya ya Uvinza mkoa wa Kigoma.

Akiwa na tabasamu na uso uliojaa matumaini, Mahmaoud hafichi hisia zake zinazowakilisha maoni ya wanakikundi wenzake, baada ya mafanikio ya kuridhisha kikundi chao kutokana na msaada waliopewa na Hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale.

Alikiri wazi kuwa msaada huo ni ukombozi kwao kwa jinsi ulivyosaidia kubadilisha utekelezaji wa majukumu yao ya uzalishaji mafuta ya mawese na ongezeko la mapato yatokanayo na shughuli hizo.

Lubugwe ni miongoni mwa vikundi vichache ambavyo vimenufaika na miradi ya uzalishaji mali inayotolewa na Hifadhi ya Taifa Mahale kama sehemu ya mpango wa ujirani mwema.

Katika kutekeleza mpango huo, Hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale ilikipatia kikundi hicho mashine tatu za kisasa kwa ajili ya uchakataji wa bidhaa zitokanazo na zao la michikichi ikiwemo kukamua mafuta ya mawese, kuvunja mise, na kukamua mafuta ya mise.



Wanakikundi wakiwa wanapatiwa mafunzo ya namna ya kutumia mashine na mtaalamu kutoka SIDO

"Mwanzoni, kabla ya kupata mashine hizi tulikuwa tunatumia muda mrefu sana katika uzalishaji. Kwa mfano, tulikuwa tunatumia siku nzima kukamua pipa mbili za mawese ambapo pia zilihitaji nguvu za wengi na muda.

"Kupitia mashine hizi, kwa sasa, tuna uwezo wa kukamua pipa moja kwa muda wa dakika 12. Kwa upande wa kuvunja mise, mtu mmoja alikuwa anaweza kuvunja debe moja tu kwa siku nzima lakini kwa sasa, ndani ya saa moja tunaweza kuvunja tani moja". Alieleza Athuman Kasongo, Katibu wa kikundi cha Lubugwe.

Alisema kuwa kutokana na ufanisi wa mashine hizo, kipato cha kikundi kimeongezeka hadi kufikia faida ya wastani wa shilingi 800,000 kwa mwezi, hatua inayosaidia wanakikundi kuwa na kipato cha uhakika.

"Mapato haya bado hatujagawana. Nia yetu ni kupata mtaji mkubwa zaidi utakaotusaidia kuwa na nguvu ya kuwekeza na kuongeza kipato chetu. Sote tumekubaliana hivyo na tunaamini tutafanikiwa, kwa msaada wa wadau wetu kama Mahale." alisisisitiza Katibu huyo.

Hata hivyo, mradi huo uliokabidhiwa kwa wanakikundi Februari, 2021, unakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zikitatuliwa, utawasaidia wanakikundi kusonga mbele kwa kasi kubwa zaidi.

Kasongo alisema kuwa kukosekana kwa umeme wa uhakika katika eneo hilo ni mojawapo ya changamoto kubwa inayosababisha kikundi kukosa mapato mengi.

" Mashine hizi zinahitaji umeme wa uhakika na hapa tunakabiliwa na changamoto hiyo, hali inayosababisha kukosa mapato kutoka kwenye mashine ya kukamua mafuta ya mise.

" Upatikanaji wa umeme wa uhakika utakiondolea kikundi na wananchi wengine adha ya ukosefu wa nishati ya uhakika na kuleta tija katika maisha yao", alisisitiza Kasongo.

Mhifadhi Mahusiano ya Jamii katika Hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale, Samwel Nassari alielezea kufurahishwa na maendeleo ya muda mfupi ya kikundi hicho na kwamba anatamani vikundi vingine viige mfano huo mzuri.

"Hakika tunajivunia kuwa na kikundi kama hiki ambacho kimedhihirisha wazi kwamba mikakati na mipango yetu ya ujirani mwema inaweza kubadilisha maisha ya watu na kuwa bora zaidi.

" Tunatamani vikundi vingine vilivyo chini ya mipango yetu ya ujirani mwema vifuate njia ya Lubugwe na siku zote, Shirika lipo tayari kushirikiana na wananchi ili wafaidi matunda ya uhifadhi" alisisitiza Nassari.



# MAPOROMOKO YA KATERELA: KIVUTIO CHA UTALII BIHARAMULO



Baadhi ya viongozi, wahifadhi na wananchi walipotembelea maporomoko

**Na Leticia Magesa**

**leticia.magesa@tanzaniaparks.go.tz**

KUANZISHWA kwa hifadhi mpya sita za taifa hivi karibuni kumesaidia kubuniwa, kutambuliwa, kuanzishwa na kuendelezwa kwa vyanzo vya utalii ambavyo awali havikupewa umuhimu wowote.

Burigi-Chato ni miongoni mwa hifadhi mpya sita zilizoanzishwa hivi karibuni ambayo ipo ndani ya wilaya tano zilizopo katika mikoa miwili ya Kagera na Geita.

Wilaya hizo ni Biharamulo, Ngara, Karagwe na Muleba katika Mkoa wa Kagera na wilaya ya Chato iliyopo Mkoa wa Geita

Mita 300 nje kutoka mpaka wa Hifadhi ya Burigi-Chato katika wilaya ya Biharamulo, kunapatikana kivutio cha utalii ambacho kikilindwa, kikitunzwa na kuendelezwa kinaweza kuwa chanzo kikubwa cha mapato kwa Halmashauri ya wilaya ya Biharamulo.

Maporomoko ya Katerela ambayo awali hayakupewa umuhimu mkubwa, sasa yanaandaliwa kupokea watalii wengi, hasa wa ndani kutokana na mandhari yake na vivutio vilivyomo kwenye eneo la maporomoko hayo.

Ni dhahiri ari mpya ya kutembelea maporomoko hayo imechangiwa kwa kiasi kikubwa na utoaji wa elimu ya uhifadhi na utalii uliofanywa na Kitengo cha Uhifadhi-Mahusiano ya Jamii cha Hifadhi ya Taifa Burigi-Chato.

Mojawapo ya shughuli zinazofanywa na Kitengo hicho ni kutoa elimu ya uhifadhi, kuboresha uhusiano kati ya hifadhi na jamii pamoja na kuhakikisha jamii inanufaika kutokana na uwepo wa hifadhi.

Katika kutekeleza madhumuni ya uhifadhi, Hifadhi ya Burigi-Chato kwa kushirikiana na viongozi wa vijiji imesaidia kutambua, kuendeleza na kuhifadhi maeneo yenye mchango mkubwa kiuchumi katika vijiji jirani

na Hifadhi. Maeneo hayo yanaweza kukuza uchumi wa kijiji iwapo yatatambuliwa, yatatunzwa na yatahifadhiwa vizuri.

Kati ya maeneo yaliyoibuliwa kuwa kivutio cha utalii ni maporomoko ya maji ya Katerela yanayopatikana katika kijiji cha Katerela, kilichopo Kata ya Ruziba, wilaya ya Biharamulo mkoani Kagera.

Maporomoko hayo ni kivutio cha utalii katika eneo hilo, kwa kuwa na mandhari ya kuvutia, hali nzuri ya hewa, uwepo wa ndege na mazingira mazuri ya kiasili.

"Maporomoko haya tumekua tukiyasimamia sisi kama kijiji. Hata hivyo, watu wanatembelea eneo hili kwa ajili ya kupumzika na kuburudika bila malipo. Kwa sasa tumeiona fursa hivyo tumebuni kuanzisha utaratibu wa malipo kwa wanaokwenda kwenye maporomoko haya ili kuongeza mapato," alisema Pudensiana Damian ambaye ni Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Katerela.

"Tupo kwenye mchakato wa kutoza kiingilio kwa sababu ni eneo la utalii. Tunasubiri majibu kutoka kwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo atupatie kibali," alisema Pudensiana na kuongeza kuwa:

" Kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa Burigi-Chato ni chachu ya kukuza utalii ndani ya hifadhi husika lakini pia na maeneo ya karibu kama maporomoko ya Katerela na watu wameanza kujifunza na kuelewa maana ya uhifadhi, utalii na faida zake".

Afisa Mtendaji huyo anaeleza kwamba wakipata kibali cha kusimamia na kutoza kiingilio kwa watalii wanaokwenda kwenye maporomoko hayo, kijiji kitawatangazia watu kupitia njia mbalimbali za matangazo ikiwamo mikutano ya hadhara.

" Tayari maofisa kutoka Hifadhini wamefika kijijini hapa kwa ajili ya kutoa elimu ya uhifadhi na utalii kwa wanakijiji na mambo yanakwenda vizuri," alisisitiza Pudensiana.

Mhifadhi katika Kitengo cha Uhifadhi -Mahusiano ya Jamii katika Hifadhi ya Taifa ya Burigi-Chato ndugu Pendaeli Shafuri alisema walitembelea maporomoko hayo kwa kushirikiana na viongozi wa kijiji hicho baada ya kuona umuhimu wa maporomoko hayo kwa uhifadhi na uchumi wa kijiji hicho na halmashauri husika.

"pamoja na mambo mengine, tulitembelea maporomoko ya Katerela, kuyaona, kutoa elimu ya uhifadhi/utalii na kuwaeleza



Mhifadhi Sharifu akiwa na viongozi wa Kijiji na baadhi ya wananchi katika maporomoko



Maporomoko na watalii wa ndani walioweza kuyatembelea

wananchi umuhimu wa maporomoko hayo, katika kukuza uchumi wa kijiji," alifafanua Shafuri.

Aliongeza kuwa jitihada hizo zimesaidia kuhamasisha na kushirikisha jamii katika kutunza maeneo hayo ya maporomoko kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

Kwa kutumia uzoefu wa wataalam wa kitengo cha mahusiano jamii cha Hifadhi ya Taifa Burigi-Chato, wananchi wa maeneo yanayozunguka maporomoko hayo wameandaliwa kutumia ipasavyo fursa zitakazopatikana kutokana na shughuli za utalii.

Fursa hizo ni pamoja na uendelezaji wa rasilimali za asili kwa ajili ya shughuli za kitalii ambazo zitaleta manufaa ya kiuchumi kwa mwananchi mmoja mmoja na jamii kwa ujumla.

Aidha, fursa hizo zitachochea ubunifu wa wanajamii kushiriki katika kazi mbalimbali za sanaa kama kutengeneza vifaa vya asili vya urembo kama shanga, vidani na mikeka kwa ajili ya kuwauzia wageni watakaotembelea maporomoko hayo.

Ni jukumu la wananchi wa Katerela na wilaya ya Biharamulo kushirikiana na Hifadhi ya Taifa ya Burigi-Chato kulinda, kuhifadhi na kusimamia maliasili waliyojaliwa kuwa nayo katika maeneo yao.



# UJIRANI MWEMA WACHOCHEA UHIFADHI NA MAENDELEO ENDELEVU QATESH



Nyumba ya watumishi katika Zahanati ya Qatesh iliyojengwa na TANAPA kwa ushirikiano na jamii

**Na Innocent Epimack**

**innocent.epimack@tanzaniaparks.go.tz**

WANANCHI wa kijiji cha Qatesh kilichopo wilaya ya Mbulu mkoani Manyara wana kila sababu ya kufurahia upatikanaji wa huduma za afya kijijini hapo baada ya kukamilika kwa ujenzi wa zahanati ya kijiji hicho.

Kukamilika kwa ujenzi wa zahanati hiyo iliyojengwa na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), kwa kushirikiana na wananchi, kumeondoa adha waliyokuwa wanapata wananchi hao ya kufuata huduma za matibabu umbali wa takriban kilomita saba hadi kijiji cha Gehandu.

Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara ilishirikiana na wananchi katika kutekeleza mradi huo ambapo hifadhi ilichangia asilimia 90 za gharama na wananchi kuchangia asilimia kumi za mradi. Mradi huo uligharimu shilingi 220 milioni ukijumuisha ujenzi wa jengo la zahanati, nyumba za watumishi pamoja na vyoo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Qatesh, Theophilo Kwaankway alieleza kukamilika kwa zahanati hiyo kuwa mkombozi kwa wananchi wa kijiji hicho na maeneo ya jirani ambao walikuwa wakilazimika kufuata huduma ya matibabu mbali na kijijini hapo.

“Kabla ya kukamilika kwa



Muonekano wa jengo la zahanati ya Kijiji cha Qatesh ambalo limejengwa na TANAPA kwa ushirikiano na jamii

zahanati hii, tulikuwa tunalazimika kutembea takriban umbali wa kilomita saba hadi Gehandu kufuata huduma za afya, na ilikuwa changamoto kubwa hasa kwa wajawazito lakini sasa huduma inapatikana hapa hapa”.

“Tunaishukuru sana TANAPA kwa kutupatia msaada huu mkubwa, na nawapongeza wananchi wenzangu wa Qatesh kwa kujitolea nguvukazi zilizosaidia mradi huu kukamilika.

“Sasa, tumeona kwa macho yetu faida ya uhifadhi na utalii.Tutashirikiana na TANAPA na mamlaka nyingine kuhakikisha tunalinda maliasili hizi kwa kudhibiti uharibifu wa mazingira, hasa msitu wa Marang’w ambao ni muhimu kwa maisha yetu na maendeleo yetu.” Alisisitiza Mwenyekiti huyo.

Mkazi wa kijiji hicho, Martha John, aliyejitambulisha kuwa mama wa watoto wanne, anaelezea furaha waliyo nayo wanawake wa kijiji hicho ambao wamekuwa wakisumbuka kwa muda mrefu kufuata huduma za uzazi Mbulu mjini.

“Kwa kweli huu ni ukombozi kwetu akina mama wa Qatesh, kwani tumeteseka sana kufuata huduma hasa ya uzazi mbali na wakati mwingine hadi Mbulu mjini. Sasa huduma zote tutapata hapa hapa labda kama ni rufaa na kwa kweli, tunapata muda wa kufanya shughuli zetu nyingine za maendeleo badala ya kutumia muda mrefu kufuata matibabu. Asante sana TANAPA,” alisema Martha

Ujenzi wa Zahanati hiyo ni utekelezaji wa mpango wa Ujirani mwema katika Hifadhi za Taifa ambao, unalenga kushirikisha wananchi waishio pembezoni mwa hifadhi katika uhifadhi na maendeleo endelevu.



# UFUGAJI NA KILIMO CHA KUHAMAHAMA TISHIO LA UHIFADHI MAHALE-KATAVI



Ukataji ovyo wa miti kwa ajili ya kufungua mashamba

**Na Francis Kone**

**francis.kone@tanzaniaparks.go.tz**

TANZANIA imebahatika kuwa na eneo kubwa linalofaa kwa kilimo, ufugaji na matumizi mengine muhimu ya mwanadamu na viumbe hai.

Bahati hiyo inatokana na uwepo wa maeneo yaliyohifadhiwa kama vile hifadhi za taifa, mapori ya akiba na misitu ya asili ambayo ni vyanzo vya maji yanayotegemewa katika matumizi mbalimbali ya viumbe hai, ikiwa ni pamoja na kilimo cha umwagiliaji.

Hifadhi ya Taifa Katavi yenye ukubwa wa Kilomita za mraba 4,471 inapatikana katika mikoa ya Rukwa na Katavi, Magharibi mwa Tanzania. Wananchi wanaoishi katika vijiji vinavyozunguka Hifadhi hii wanajishughulisha na shughuli za kilimo, ufugaji nyuki, uvuvi, ufugaji wa ng'ombe na biashara.

Katika siku za karibuni, wakulima na wafugaji kutoka Mikoa ya Simiyu, Shinyanga, Mwanza na Tabora wamehamia kwa wingi katika wilaya za Nkansi na Tanganyika mkoani Katavi.

Wakulima hao ambao pia ni wafugaji, ni hodari katika uzalishaji mazao ya chakula na biashara lakini wana mfumo usio rafiki kwa mazingira kutokana na utaratibu wao wa kuhamahama.

Kwa mfano, wakulima hao hulima eneo moja kwa miaka

miwili au mitatu na kisha hulitelekeza na kwenda kufyeka pori au msitu katika eneo lingine jipya lenye rutuba.

Aina hii ya kilimo inayofanywa na jamii hizo imesababisha athari mbalimbali, zikiwemo maji kukauka/kupungua katika Mto Katuma ambao ni muhimu na tegemeo kwa wanyamapori na binadamu, pia ni moja ya vyanzo vya maji katika Ziwa Rukwa.

Kilimo na ufugaji wa kuhama hama ni tishio la uwepo wa ushoroba unaotegemewa na wanyamapori katika mfumo wa Ikolojia wa Mahale Katavi. Mto Katuma ni chanzo muhimu cha maji katika Hifadhi ya Taifa Katavi kinachotegemewa na wanyamapori pamoja na matumizi ya binadamu ikiwemo kilimo cha umwagiliaji.

Hifadhi ya Taifa Katavi pamoja na wadau wengine ikiwa ni pamoja na Halmashauri za wilaya, The Nature Conservancy (TNC) na Frankfurt Zoological Society (FZS) wamefanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha Mto Katuma unahifadhiwa. Miongoni mwa jitihada hizo ni kutoa elimu ya uhifadhi, kugawa miche ya miti na kuwezesha uaandaaji wa matumizi ya ardhi kwa jamii hizi.

Hifadhi kupitia Kitengo cha Uhifadhi-Mahusiano ya jamii, imefanikiwa kutoa elimu ya uhifadhi kwa wajumbe wa serikali za vijiji jirani, mikutano ya hadhara, Baraza la maendeleo la kata (WDCs), shuleni na katika vikundi mbalimbali vilivyotembelea hifadhi. Elimu hii ilijikita kueleza athari za uharibifu wa mazingira, yakiwemo ya Mto Katuma ambao unaweza kukauka na kuhatarisha maisha ya viumbe hai wanaotegemea mto huo.

"Tumefanikiwa kugawa miche 1,600,000 ya aina ya msonobari (pine) kwa wananchi kwa ajili ya kurejesha uoto asili wa Mto Katuma. Tumefuatilia miti hiyo kwa jamii ili kujua ustawi wake. Zaidi ya asilimia 85 ya miti tuliyogawa imeota na ina maendeleo mazuri." alieleza Lucy Mlagala, Afisa Ufuatiliaji na Tathimini kutoka Shirika la TNC

Aidha, halmashauri ya wilaya ya Tanganyika ilishirikiana na wadau wa uhifadhi ili kupata namna ya kutatua changamoto ya kilimo na ufugaji wa kuhamahama kwa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi.

"Katika wilaya ya Tanganyika, FZS imefanikiwa kuwezesha uandaaji wa mpango wa matumizi ya ardhi kwa vijiji 16 jirani na Hifadhi ya Katavi. Kupitia mipango hii tuna matarajio kuwa wananchi wataacha kilimo cha kuhamahama na pia ushoroba wa wanayamapori wa Mahale-Katavi utakuwa salama".

"Katika hatua yingine, tumewezesha kurekebisha vizuizi vya maji yanayochepushwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji mpunga ili kudhibiti matumizi holela ya maji." alieleza Regina Domoko, Afisa kutoka Shirika la FZS Mpanda.

"Kijiji kinapokuwa na mpango wa matumizi ya ardhi huwezesha upangaji mzuri wa maendeleo kwa watumiaji wote wa ardhi bila kuathiri shughuli zao. Jambo muhimu ni wanakijiji kuhakikisha wanasimamia mpango waliokubaliana na kutekeleza sheria ndogo," alisisitiza Janeth Bundala, Afisa Wanyamapori wilaya ya Tanganyika.

" Wakulima hawataweza kuendelea na kilimo cha kuhamahama kwa sababu maeneo ya kilimo yameshatambuliwa katika vijiji na hatutavumilia uharibifu wa mazingira na misitu," alisisitiza Janeth.



# RHOBI: NYOTA ANAYETUMIA SANAA YA UIMBAJI KUHAMASISHA UHIFADHI SERENGETI



Bi. Rhobi akitoa elimu kwa wanafunzi

**Na Zablon Mtweve**

**zabron.mtweve@tanzaniaparks.go.tz**

HIFADHI ya Taifa Serengeti sasa inatumia vijana wanaoishi jirani na hifadhi katika kutoa Elimu ya Uhifadhi.

Utaratibu huo ulianza mwaka 2021, ukiwa na lengo la kuboresha utoaji wa elimu ya uhifadhi kwa kutumia vijana waliochaguliwa na vijiji vyao. Lengo la kutumia vijana hao ni kupanua wigo wa utekelezaji wa Mpango wa Ujirani Mwema wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Mhifadhi Mahusiano Jamii katika Hifadhi ya Taifa Serengeti, Robert Masobeji anaamini matumizi ya vijana hao yatasaidia sana kuwaelimisha zaidi wakazi wa vijiji vyao ambao ni wadau wakubwa wa uhifadhi kwa muda mrefu.

“Jumla ya vijana 18 kutoka vijiji 16 katika wilaya za Serengeti, Tarime, Bunda na Bariadi wameanza kutekeleza mbinu hiyo ambayo imeonyesha kuwa na mafanikio katika umahasishaji na utoaji elimu ya uhifadhi.

Kutokana na umahiri mkubwa wa kuhamasisha jamii kuhusu uhifadhi wa maliasili na mazingira, vijana hawa waliochaguliwa kwa kufuata miongozo ya TANAPA ya kutumia wanajamii wenye sifa

katika kutoa eimu ya uhifadhi kwa wenzao, watatusaidia sana kwani wanatumia lugha rahisi na inayoeleweka vyema kwa wenyeji."alieleza Mhifadhi Masobeji.

Baadhi ya sifa zilizozingatiwa kuwapata vijana hao ni pamoja na kuwa mkazi wa kijiji husika, awe amehitimu kidato cha nne, asiyejihusisha na ujangili, anayekubalika katika jamii yake na mwenye mwenendo mzuri.

Rhobi Mwita Mahando ni mmoja wa vijana hao 18 waliochaguliwa ambaye ameonyesha jitihada za kipekee katika kuhamasisha jamii kuhusu uhifadhi kupitia makundi mbalimbali ya kijamii kijijini Nyamburi wilaya ya Serengeti.

Baada ya kupewa mafunzo yaliyowezeshwa na TANAPA kupitia Hifadhi ya Taifa Serengeti, Rhobi alianza kutekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na uongozi wa kijiji chake na kata.

Katika kipindi kifupi cha kuanzia Julai hadi Septemba 2021, Rhobi amefanikiwa kutoa elimu ya uhifadhi kwenye shule ya msingi Nyamburi na shule ya sekondari Nyamburi. Vile vile, ametembelea nyumba 4 za ibada na kushiriki vikao 3 vya Serikali ya kijiji pamoja na mikutano 6 ya hadhara ya vitongoji na kuwafikia watu 1,768. Pamoja na mbinu nyingine, Rhobi ameweza kufanikiwa katika kutoa elimu ya uhifadhi kupitia kipaji chake cha uimbaji alichonacho.

Katika kipindi kifupi, Rhobi amedhihirisha kuwa nyota yake inakubalika kutokana na jinsi anavyojituma kwa wanajamii akiwa bado na umri mdogo kwa wanajamii wa rika zote (Esaigha) katika kijiji chake.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nyamburi, Joshua Obwago anazungumzia kipaji cha binti huyo kuwa ni cha kipekee na kinachopeleka ujumbe haraka, na kwa jinsi ulivyokusudiwa.

"Anatumia lugha rahisi inayoeleweka kwa jamii yake na ndio maana anakubalika kila mahali, kwa marika yote wawe wazee, vijana na hata wanawake wenzake. Ni hazina tunayopaswa kuilea na kuitunza kwa faida ya uhifadhi na mazingira," analisisitiza na kuongeza: "Kwa kutumia ubunifu na kipawa chake, Rhobi huwa anaomba vipindi shuleni au kwenye nyumba za ibada ili kutumia sanaa yake kuelezea umuhimu wa uhifadhi na Hifadhi ya Taifa Serengeti. Hapa shuleni tumempangia vipindi kama mmoja wa waalimu wa hifadhi Maliasili na Mazingira."

Naye Afisa Mtendaji wa Kata ya Sedeco,Charles Tiganga anaunga mkono utumiaji wa mbinu hizo za uhamasishaji uhifadhi akisema kwamba zinafikisha ujumbe kwa watu wengi na kwa kutumia muda mfupi.

"Hakika mbinu hii ya kuwatumia wanajamii katika kutoa elimu ya Uhifadhi imetoa hamasa kubwa kwa vijana na jamii katika suala zima la uhifadhi wa maliasili na mazingira. Pia kupitia mbinu hii inawafanya vijana na jamii kuona kuwa wao ndio wamiliki wa hizi rasilimali na kuongeza ari ya kuzilinda, tofauti na jinsi wengi wanavyoona hizi Hifadhi kuwa ni mali ya TANAPA," alibainisha Tiganga na kuongeza:

"Mpango huu ni mzuri kwetu kwa sababu unatuwezesha kujua faida za hifadhi na kupata elimu zaidi ya mambo ya maliasili. Wanajamii waliona kuwa Hifadhi iko kwa ajili ya viongozi tu na ni kama haiwahusu, ila kupitia mpango huu, kwa kweli wananchi sasa wanaona hifadhi ni ya kila mtu. Mpango huu pia utasaidia kuondoa mtazamo hasi kuhusu uhifadhi na kuboresha mahusiano".



# RUMANYIKA-KARAGWE YAWAFUNDA MGAMBO UHIFADHI KUCHOCHEA ULINZI WA MALIASILI



Afisa Mhifadhi Fadhili Iddi akitoa elimu ya uhifadhi kwa wanamgambo

**Na Fadhili Iddi**

**fadhili.iddi@tanzaniaparks.go.tz**

HIFADHI ya Taifa Rumanyika-Karagwe imetumia mafunzo ya mgambo yanayotolewa kwa vijana wilayani Kyerwa Mkoa wa Kagera kutoa elimu ya uhifadhi ili washiriki katika ulinzi wa maliasili katika maeneo yanayozunguka hifadhi hiyo.

Mafunzo hayo yaliyoshirikisha vijana wakakamavu 78, yalitumika kufikisha elimu ya uhifadhi ambayo itatumiwa na wanamgambo hao kulinda rasilimali zilizo katika maeneo yao.

Mhifadhi wa Ulinzi katika hifadhi hiyo, Upendo Massawe alisema kuwa jukumu la kutoa elimu ya uhifadhi wa maliasili na sheria zake kwa wanamgambo ni njia muhimu na mahususi katika kuboresha uhifadhi wa maliasili na kupunguza ujangili ndani na nje ya Hifadhi pamoja na kuboresha mahusiano kati ya Hifadhi na Jamii.

Alifafanua kwamba Jeshi la Mgambo kihistoria lilianzishwa kwa mujibu wa sheria mwaka 1963 na majukumu yake yamefafanuliwa katika Sheria ya Ulinzi wa Taifa Tanzania ya mwaka 1966 kifungu namba 19 kifungu kidogo cha (11b). Baadhi ya majukumu hayo ni kufanya kazi na taasisi za Serikali katika kusimamia ulinzi na usalama, kutekelezwa kwa sheria za nchi na kutoa msaada kwa Serikali wakati wa dharura.

Vijana hao 78 waliopatiwa mafunzo ya mgambo wilayani humo kupitia Mshauri wa Jeshi la Akiba, wanatoka katika tarafa ya Nyakatuntu vijiji vinne vya Rwabigaga, Kamuli, Kyerere na Nyakatuntu vilivyo jirani na Hifadhi.

" Ni katika mafunzo hayo, uongozi wa Hifadhi ya Taifa Rumanyika-Karagwe ulitumia fursa hiyo kufanya mafunzo ya elimu ya uhifadhi kwa mgambo hao ambao mbali ya jukumu lao la kulinda rasilimali, lakini pia watakuwa mabalozi wa uhifadhi katika maeneo yao,"



Baadhi ya washiriki wa semina ya elimu ya uhifadhi katika picha ya pamoja wakifurahi jambo

anaeleza Mhifadhi Upendo

Mada zilizowasilishwa, kwa mujibu wa Mhifadhi Upendo, ni pamoja na Muundo wa jeshi la Uhifadhi, Maeneo yaliyohifadhiwa Tanzania, Faida za uhifadhi, Sheria za Hifadhi za Taifa, Ujirani mwema, Ujangili na nyara za serikali, Uvuvi haramu, Migongano baina ya wanyamapori na binadamu na Ulinzi shirikishi.

Aidha, mafunzo hayo yalijikita katika kuonyesha namna vijana hao wanavyoweza kushiriki katika ulinzi wa maliasili za nchi katika maeneo yao.

" Hii ni kutokana na ukweli kwamba mgambo wamepewa jukumu hilo kisheria na wapo mstari wa mbele katika kusimamia utekelezwaji wa sheria kwa kushirikiana na serikali na wadau wengine," alisisitiza Mhifadhi Upendo.

Hifadhi ya Taifa Rumanyika-Karagwe inatarajia kuwa vijana hawa waliopata mafunzo watasiadia kusimamia sheria za Uhifadhi wa maliasili na kuchochea uhifadhi endelevu kwa kufikisha kwa jamii elimu waliyoipata katika ngazi mbalimbali ikiwemo kwenye familia zao na vijiweni.

"Vijana hao pia wanatarajiwa kutoa taarifa za uhalifu na kupambana na wanyamapori wakali na waharibifu katika vijiji vyao," alifafanua na kuungwa mkono na mmoja wa wakufunzi wa mafunzo hayo ya mgambo Koplo Deomedes Rupia kwa kuongeza:

"Mafunzo yaliyotolewa ni muhimu katika kuchochea uhifadhi katika maeneo ya vijiji jirani na Hifadhi ambapo Mgambo wanatarajiwa kufanya kazi zao za kila siku".

Koplo Rupia alieleza kuwa mafunzo ya uhifadhi ni hatua muhimu katika kuwapa maarifa mgambo yatakayowasaidia kutambua na kusimamia sheria za maliasili katika maeneo yao. Hata hivyo, alitoa Rai kuwa vijana hao wenye ari na nia wanatakiwa kupatiwa mafunzo zaidi na kushirikishwa wakati wa uundaji wa vikundi vya ulinzi shirikishi vya kulinda maliasili.

TANAPA inapenda kuwaalika wadau mbalimbali kuwezesha mafunzo zaidi kwa mgambo hao ili kuwaongezea weledi katika utendaji wao. Katika kufanya hivyo kutawezesha kutekeleza kwa vitendo kauli mbiu ya Wizara ya Maliasili na Utalii inayosema kuwa "Tumerithishwa, tuwarithishe".

# UHIFADHI KUPITIA HADITHI

## KISA CHA BABA NA MAMA MAUA: MFANO WA SULUHISHO LA MIGOGORO KATI YA JAMII NA HIFADHI.

**Theones Kagwebe na Fadhili Iddi.**

**fadhili.iddi@tanzaniaparks.go.tz**

SIKU moja Baba na Mama Maua walikuwa wameketi mezani wakila chakula cha usiku. Wakati wakiendelea kupata mlo, ghafla panya alikatiza kutoka upande aliokaa Mama Maua kuelekea upande aliokaa Baba Maua. Ingawa Baba Maua hakumuona panya huyo, ila alihisi kuna kitu kimekatiza bila kutambua uelekeo wake.

Tukio hilo lilianzisha mjadala kati ya wawili hao kama ifuatavyo:-

**Mama Maua:** "Baba Maua kuna panya amekatisha hapa, umemuona?"

**Baba Maua:** "Sijamuona, ila nimehisi kuna kitu kimekatiza kutoka upande wangu''

**Mama Maua:** "Ni panya amekatiza Baba Maua na katokea upande niliokaa mimi"

**Baba Maua:** "Kumbe ni panya ?"

**Mama Maua:** "Kesho tununue dawa ya panya tuweke upande huu alipotokea"

**Baba Maua:** "Hapana, tuweke upande huu wangu, ndipo alipotokea ''

**Mama Maua:** "Baba Maua mwongo wewe, katoka upande wangu kuja kwako"

**Baba Maua:** "Wewe mwanamke, katoka upande wangu kuja upande wako"

**Mama Maua:** "Jamani. We mbishi kama mama yako"

**Baba Maua:** "Alaa, nilishakwambia usinitukanie mama yangu wewe mwanamke"

(Kwa hasira, Baba Maua alimtolea mkewe matusi ya nguoni kitu ambacho kilizua zogo kati ya pande hizo mbili na kusababisha baba Maua kumpiga mkewe kibao. Mama Maua alipiga yowe ambalo liliwashitua majirani. Jirani mmoja anayefahamika kwa jina la Mzee Chaupole alifika na kugonga mlango wa nyumbani kwa Baba na Mama Maua.

**Mzee Chaupole:** "Jirani! jirani! Kulikoni? hebu naomba nifungulie mlango, mimi Mzee Chaupole"

(Baba na Mama Maua walivyosikia sauti ya Mzee Chaupole ambaye ni mtu anayeheshimika katika kijiji chao, waliacha zogo huku wakihema kutokana na hasira na purukushani iliyokuwa ikiendelea)

**Baba Maua:** "Mzee Chaupole hamna kitu, we nenda kalale bwana"

**Mama Maua:** "Mzee Chaupole, huyu mwanaume mkorofi sana"

**Mzee Chaupole:** "Nakuomba unifungulie jirani tuyasuluhishe. Haina haja ya kugombana nyie ni watu wazima."

(Baba Maua alimsikia tena Mzee Chaupole aliyekuwa akiongea kwa sauti ya upole iliyofanya hasira zake kuyeyuka kama pande la barafu juani na kuamua kufungua mlango)

**Baba Maua:** "Karibu Jirani, ingia ndani"

(Huku akilia kutokana na zogo lililokuwa linaendelea)

**Mama Maua:** "Shikamoo Mzee Chaupole"

**Mzee Chaupole:** "Marhaba mama! Pole! hebu nyamaza kwanza, tuongee."

(Wote watatu walienda na kukaa kwenye meza iliyokuwa ikitumiwa na Baba na Mama Maua).

**Mzee Chaupole:** "Haya niambie kulikoni! ugomvi wa nini? Zogo lenu linasikika hadi huko kwa majirani"

**Mama Maua:** "Mzee Chaupole, huyu mwanaume mkorofi sana, kunipiga na kunitukana kote huko ni kutokana na kumueleza ukweli. Mimi nimemuona panya akikatiza kutokea upande niliokuwa nimekaa nikamwambia tununue dawa tuweke sehemu alipotokea panya. Yeye kawa mbishi na kuanza kunitukana matusi ya nguoni na kunipiga."

**Baba Maua:** "Nishakwambia nyamaza we mwanamke, Panya alitokea upande niliokua nimekaa mimi, na kilichofanya umtusi mama yangu ni nini? Ee ni nini?"

(Baba Maua aliamka kwa hasira na kutaka kumpiga mama Kenge lakini Mzee Chaupole alimtuliza na kumsihi akae chini waongee)

**Mzee Chaupole:** "Nawaomba mpunguze hasira zenu ili tuongee na tufikie muafaka. Ugomvi haujawahi kuwa suluhisho hata mara moja. Kuna usemi wa wahenga unasema "hasira hasara, hivyo naomba mnisikilize."

(Baba na Mama Maua walikaa kwa makini na kumsikiliza Mzee Chaupole).

**Mzee Chaupole:** "Nimewasikia wote vizuri. Je, lengo lenu wote si ilikuwa kununua sumu ili kumuua panya anayeleta uharibifu kwenye nyumba yenu?"

**Mama Maua:** "ndio Mzee Chaupole"

**Baba Maua:** "ndio"

**Mzee Chaupole:** "kama hivyo ndivyo, hakukuwa na haja ya kugombania panya kaonekana kutoka upande upi. Mnatakiwa kutambua kwamba licha ya kutofautiana upande alipotokea panya, lakini panya huyo yupo kwenye nyumba yenu.

"Kwenye ugomvi wowote watu wanatakiwa kuangalia vitu wanavyokubaliana badala ya vile wanavyotofautiana. Baba Maua hutakiwi kutumia mabavu na matusi kumaliza tofauti zako na mkeo. Na wewe Mama Maua hutakiwi kutumia maneno ya kumuudhi mwenzako ili kutetea unachokiamini. Ona sasa panya kasababisha ugomvi kwenu na huenda anaendelea na uharibifu kwenye nyumba yenu. Nyie mnagombana lakini tatizo la panya bado lipo pale pale."

Baba na Mama Maua waliyasikiliza kwa makini maneno ya Mzee Chaupole na kugundua hawakuwa na haja ya kugombana.

**Baba Maua:** "Kweli Mzee Chaupole. Hakukuwa na haja ya kugombana na mke wangu. Nisamehe Mama Kenge."

**Mama Maua:** "Nimekusamehe mume wangu. Na wewe nisamehe kwa maneno yangu yaliyokuudhi"

**Baba Maua:** "Usijali mke wangu. Kesho nitanunua sumu ya panya na tutaweka sehemu zote panya wanapoweza kujificha"

**Mama Maua:** "Sawa Baba Maua. Tutashirikiana kuweka sumu ya panya ili tulimalize tatizo hili nyumbani kwetu."

**Mzee Chaupole:** "Hivyo ndivyo inatakiwa kushughulikia matatizo yetu. Nashukuru mmeelewana, na muwe na amani maana penye amani, suluhisho la matatizo mengi hupatikana. Haya jamani kwaherini na usiku mwema."

**Baba Maua:** "Kwaheri Mzee Chaupole. Tunashukuru kwa busara zako"

**Mama Maua:** "Asante Mzee Chaupole. Uende salama"

**Mahudhui ya Hadithi**

Kisa hiki kinatufundisha kwamba, migogoro mingi inashindwa kutatuliwa kwa sababu kila upande unajiona uko sahihi huku ukilazimisha kile wanachokiamini ndio kiwe suluhisho. Hali hii, inatokea sana kwenye migogoro kati ya hifadhi na jamii ambapo kila upande unaamini kile wanachokijua na kukitaka kiwe ndio njia pekee ya kumaliza mgogoro uliopo.

Tunajifunza kwamba kila mmoja aking'ang'ania kuwa sahihi bila majadiliano migogoro huongezeka.

Aidha, tumeona kwamba tunapokuwa na mgogoro na tukashidwa kuelewana ni vyema kutafuta msuluhishi atakayewezesha kufikia muafaka kama alivyofanya Mzee Chaupole. Pia kunapokua na amani baina ya pande zinazozozana na kutokuwa kwenye jazba, suluhu hupatikana kirahisi na hivyo mgogoro kutatuliwa.

# SAANANE YATUMIA MICHEZO KUHAMASISHA ELIMU YA UHIFADHI




Mkuu wa Hifadhi wa Kisiwa cha Saanane ACC. Eva Malya akitoa maelezo ya bonanza

**Na Sadick Mohamed**

**sadick.mohamed@tanznaiparks.go.tz**

MICHEZO ni moja ya njia muhimu inayoweza kufikisha ujumbe kwa hadhira kubwa kwa wakati mmoja kutokana na kupendwa na watu wa rika mbali mbali katika jamii.

Kwa kutambua umuhimu wa michezo, Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Saanane kupitia kitengo cha Uhifadhi-Mahusiano ya Jamii kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali linaloitwa Home Life Sport hivi karibuni iliamua kutumia njia ya michezo kufikisha ujumbe wa uhifadhi kwa jamii kupitia



Wachezaji wakiwa katika mchezo wa mpira wa wavu

mashindano ya mpira wa wavu yaliyopewa jina la Saanane Island Volleyball Championships.

Mashindano hayo, yalitumika kufikisha ujumbe mahsusi wa umuhimu wa uhifadhi kwa washiriki zaidi ya 700 kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na hotuba kiwanjani, mabango ya uwanjani, jezi zenye ujumbe wa uhamasishaji, vipeperushi na mitandao ya kijamii pamoja na vyombo vya habari kama Radio Jembe FM na Star TV.

Katika uzinduzi wa mashindano hayo, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi Eva Mallya ambaye ni Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Saanane alieleza lengo la mashindano hayo kuwa ni pamoja na: ***"Kutoa elimu ya uhifadhi ili kuiwezesha jamii kushiriki kikamilifu kutunza mazalia ya samaki na viumbe wa majini, kutunza wanyamapori waliopo kwenye kisiwa hicho na kulinda Ikolojia ya kisiwa hicho kwa ujumla."***

Washiriki wa mashindano hayo pamoja na watazamaji waliojitokeza kwa wingi walipata elimu ya uhifadhi



Wanamichezo wakipeana dondoo kabla ya kuanza kucheza

kupitia mada mbalimbali zilizowasilishwa kuhusu umuhimu wa wananchi kutunza mazingira yao kuanzia ngazi ya familia na athari za uharibifu wa mazingira kwa jamii husika.

Katika kuhakikisha hamasa na ari kwa washiriki wa michezo, zawadi mbalimbali zilitolewa kwa mshindi wa kwanza na wa pili. Mshindi wa kwanza alipewa Kombe, Jezi zilizo na nembo ya TANAPA na Jina la Hifadhi na ujumbe wa uhifadhi, Fedha taslimu shilingi laki moja (100,000) na kupewa fursa ya kutembelea Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Saanane bure.

Mshindi wa pili alipewa zawadi ya Jezi yenye nembo ya TANAPA na Jina la Hifadhi ikiwa na



Wanamichizo wakiwa katika mchezo

ujumbe wa uhifadhi na fedha taslimu shilingi elfu hamsini (50,000)

Kamishna Msaidizi Eva alieleza kuwa baada ya mashindano hayo anatarajia kuona jamii ikishiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi ikiwa ni pamoja na kupungua kwa ujangili wa samaki na uchafu kwenye mialo, na pia wananchi watakua tayari kutoa taarifa za viashiria vya uhalifu.

# MATUNDA YA ULINZI SHIRIKISHI YAANZA KUONEKANA RUAHA



Baadhi ya wanakikundi cha ulinzi shirikishi kutoka wilaya ya Chamwino Dodoma

**Na Shariff Abdul**
**shariff.abdul@tanzaniaparks.go.tz**

ULINZI shirikishi ni mpango wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) unaolenga kushirikisha jamii katika kutunza na kulinda maliasili zilizopo ndani na nje ya Hifadhi za Taifa 22 zilizopo nchini.

Katika Hifadhi ya Taifa Ruaha, mpango huu ulianzishwa na kuzinduliwa katika vijiji vitatu vya Chinugulu, Manda na Ilangali vilivyopo wilayani Chamwino Mkoa wa Dodoma

Katika vijiji hivyo, Vijana 102, wakiwemo wanaume 88 na wanawake 14 walikua tayari kujitolea kwa hiari kulinda maliasili katika vijiji vyao baada ya kupatiwa mafunzo ya ulinzi shirikishi.

Kila kijiji kina kikundi kimoja ambapo kijiji cha Manda kuna jumla ya wanakikundi 43, Ilangali 30 na Chinugulu 29.

Shughuli zinazofanywa na vikundi hivi ni pamoja na doria katika maeneo yao ya vijiji pamoja na kushirikiana



Sehemu ya mizinga 120 iliyotolewa na TANAPA kwa vikundi vya Manda, Ilangali na Chinugulu wilaya ya Chamwino

na Askari kutoka Hifadhi ya Taifa Ruaha na kikosi dhidi ya ujangili (KDU) katika maeneo yanayosimamiwa na TANAPA na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA).

"Mara nyingi tumekuwa tukipata ushirikiano mzuri kutoka Hifadhi ya Taifa Ruaha pamoja na TAWA tunapofanya nao kazi katika maeneo yetu na hata maeneo yao.

Pamoja na mafanikio tuliyoyapata, kuna changamoto zinatukabili ikiwemo baadhi ya wananchi kutuchukia kwa vile tunawazuia kuvuna maliasili bila kuwa na kibali. Hawa watu walishazoea kuvuna hizi mali kiholela, wanatuona sisi tunawazibia riziki zao. Tunashukuru wananchi na Serikali ya kijiji (Chinugulu) wameelewa na wameendelea kutupa ushirikiano katika kazi tunazofanya. Hii inatutia moyo wa kuendelea na hii kazi" alisema Gozbert Masile, mkuu wa kikosi cha ulinzi shirikishi kijiji cha Chinugulu.

Mkuu huyo wa Kikosi cha Ulinzi Shirikishi kijijini hapo alisema kuwa majukumu mengine ya kikundi hicho ni kushiriki katika kukabiliana na wanyamapori waharibifu wanapotokea katika vijiji vyao.

Kiongozi wa kikundi kingine kilichopo katika kijiji cha Ilangali, Baraka Matonya alisema kuwa anajivunia kuwa na kikosi kinachoshiriki kikamilifu kulinda maliasili na kuwadhibiti wanyamapori waharibifu wanaovamia kijijini.

"Kazi hii ya ulinzi shirikishi pamoja na changamoto

zake, inafaida nyingi ikiwemo kupunguza vitendo vya uchomaji mkaa katika vijiji vyetu kwani ilikuwa imekithiri sana. Ili tupate mafanikio zaidi, tunahitaji ushirikiano kutoka kwa viongozi wa vijiji na kata, wananchi na wadau wengine ikiwemo TANAPA, TAWA na Mashirika mengine watuwezeshe zaidi na kutupatia mafunzo ya mbinu bora zaidi za ufanyaji kazi," alisema Matonya

"Pia tumekuwa mstari wa mbele kukabiliana na wanyamapori waharibifu haswa Tembo ambao mara kwa mara wamekuwa wakifika katika maeneo yetu na kufanya uharibifu wa mazao. Tulipatiwa mafunzo na Hifadhi ya Ruaha ya namna ya kukabiliana na wanyamapori hawa (Tembo), kwa sababu hali ilikuwa mbaya sana. Tembo wanaweza fika wakala mazao shambani, na wakati mwingine wakaharibu ghala na kula mahindi yaliyohifadhiwa". aliendelea kueleza Matonya

Kwa mujibu wa taarifa ya vikundi hivyo, tangu vianzishwe mwaka 2014, vimefanikiwa kukamata majangili 59, vipande 6 vya meno ya tembo, gobore 19, mbao 834, mifugo (ng'ombe na mbuzi) 2,500, baruti yenye uzito wa gramu 510, nyavu 150 za uvuvi, mitumbwi 17, fataki 6, bangi vifurushi 45, mitego ya waya 2, nyara za wanyamapori 50, misumeno 2 na vifurushi 335 vya mkaa.

Utoaji wa motisha kwa vikosi hivi ulibuniwa kwa kuzingatia sheria ndogo za vijiji. Asilimia 50 ya faini zinazotokana na vitu vilivyokamatwa hutolewa kwa vikosi vya ulinzi shirikishi vilivyohusika na ukamataji. Hata hivyo, TANAPA imeboresha mpango huo kwa kuviwezesha vikundi hivyo mradi wa kuzalisha na kukuza kipato kwa ufugaji nyuki. Katika mwaka huo, jumla ya mizinga 120 ya kisasa pamoja na mafunzo ya ujasiriamali vilitolewa.

Mradi huu wa ufugaji nyuki pamoja na kuwapatia wanakikundi kipato, pia ulilenga kuwezesha utunzaji wa misitu katika vijiji kwani ni moja ya shughuli ambazo ni rafiki kwa mazingira. Moja wapo ya mafanikio ya mradi ni pamoja na wanakikundi kufanikiwa kuvuna asali lita 640 katika mwaka 2021.

Pamoja na mafanikio waliyopata, vikundi hivi vinakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo wakipatikana wadau wengine wa uhifadhi wanaweza kuwasaidia katika kuzitatua. Changamoto hizo ni pamoja na ukosefu wa mafunzo ya mara kwa mara, vitendea kazi bora ikiwemo GPS, sare na viatu, makoti ya mvua pamoja na kuwezesha miradi mingine zaidi ya ujasiriamali itakayowawezesha kupata kipato mbadala na kutoa hamasa na motisha kwao.

# TANAPA kuwatumia Walimu na waelimisha jamii kutoa elimu ya uhifadhi



Washiriki wa mafunzo ya waelimishaji jamii katika Hifadhi ya Serengeti

**Na Godwell Ole Meing'ataki**

**godwell.meingataki@tanzaniaparks.go.tz**

Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) kupitia Kitengo cha Uhifadhi-Mahusiano ya Jamii lina jukumu la kutoa elimu ya uhifadhi kwa jamii zinazoishi jirani na Hifadhi. Lengo la kutoa elimu hii ni kukuza uelewa wao kuhusu mambo mbalimbali ya kiuhifadhi kama vile athari za ujangili, faida za uhifadhi na namna wanavyoweza kushirikiana na TANAPA katika kuhakikisha uhifadhi endelevu.

Mpango wa ujirani mwema ulianzishwa mwaka 1988 katika vijiji vitatu ambavyo ni Ololosokwan, Soitsambu na Oloipiri katika Wilaya ya Ngorongoro mashariki mwa Hifadhi ya Taifa Serengeti.

Mpango huu ulitokana na kikao cha wadau kilichofanyika mwaka 1985 kutafuta ufumbuzi wa tatizo la ujangili wa tembo, nyati, faru na wanyama wengine uliokuwa umekithiri katika Hifadhi ya Taifa Serengeti

licha ya kuwepo kwa sheria na ulinzi madhubuti. Kikao kiliazimia kuwashirikisha wanajamii wanaoishi jirani na Hifadhi katika kupambana na ujangili.

Matokeo mazuri yaliyotokana na vijiji vya mfano yaliifanya TANAPA mwaka 1994 kuanzisha idara ya Ujirani Mwema (ambayo sasa ni kitengo cha Uhifadhi-Mahusiano ya Jamii) ambayo ilikuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa, vijiji vyote vinavyopakana na Hifadhi za Taifa Tanzania vinafikiwa na elimu ya Uhifadhi ili kupunguza ujangili pamoja na kuboresha mahusiano baina ya vijiji na Hifadhi.

Kupitia kitengo cha Uhifadhi-Mahusiano ya Jamii kwa muda mrefu, TANAPA imekuwa ikitoa elimu ya uhifadhi katika vijiji/kata/wilaya/mkoa jirani kwa kutumia njia mbalimbali kama vile mikutano mikuu ya vijiji, Halmashauri za vijiji, michezo, ziara za kutembelea hifadhi, kushiriki katika mikutano, semina, warsha na matamasha mbalimbali.

Licha ya jitihada zote zilizofanywa na TANAPA kutoa elimu ya uhifadhi kwa jamii, kumekuwa na changamoto ya kutofikia jamii yote kwa wakati kutokana na uhaba wa watumishi ikilinganisha na maeneo makubwa ya kufanyia kazi.

Ili kutatua changamoto hiyo, hivi karibuni, TANAPA imeanzisha program ya majaribio ya kutoa elimu ya uhifadhi katika Hifadhi za Taifa 12 kwa kutumia waelimishaji jamii na walimu wa masomo ya Maarifa ya Jamii darasa la tano kwa shule za msingi na Jiografia kidato cha pili kwa shule za sekondari ili upanua wigo wa utoaji elimu na kuwafikia watu wengi zaidi.

Utekelezaji wa kutumia waelimishaji jamii kutoka vijiji jirani umeanza kufanyika katika hifadhi za Taifa Serengeti na Ruaha ambapo jumla ya vijiji 31 kati ya 263 vinavyopakana na Hifadhi hizo vimefikiwa. Jumla ya watu wapatao 60,966 wamefikiwa na elimu ya uhifadhi katika vijiji hivyo kwa kipindi cha Julai-Desemba 2021 kupitia mikutano mikuu ya vijiji, mikutano ya Halmashauri za vijiji, kutembelea makundi mbalimbali vijijini, kushiriki katika maonyesho, michezo, sherehe pamoja na mikusanyiko ya dini.

Vilevile, Hifadhi za Taifa 10 zimeanza utekelezaji wa program hiyo kwa kutumia walimu wa somo la Jiografia kwa kidato cha pili katika shule 43 na waalimu wa somo la Maarifa ya Jamii kwa darasa la tano katika shule 104. Hifadhi hizo ni Saadani, Mikumi, Udzungwa, Kitulo, Katavi, Mahale, Gombe, Rubondo, Ibanda-Kyerwa na Rumanyika-Karagwe. Jumla ya wanafunzi 19,940 wamefikiwa kupitia vipindi vya darasani na pia katika klabu za mazingira kwa kipindi cha Julai-Desemba 2021.

TANAPA inaamini kuwa kama wanafunzi wa shule za Msingi na Sekondari wataelimishwa kuhusu masuala ya uhifadhi wangali shuleni, itaweka msingi mzuri wa kufikia uhifadhi endelevu.

Aidha, kupitia program hiyo watu wengi zaidi watafikiwa na elimu ya uhifadhi katika namna bora ya mawasiliano ambayo itawezesha maelewano miongoni mwa wanajamii na kuimarisha uhifadhi wa maliasili katika Hifadhi za Taifa. Baada ya kukamilisha program ya majaribio kwa ufanisi, programu hii itaendelea kufanyika katika Hifadhi zingine ili kuhakikisha kuwa elimu ya Uhifadhi inawafikia wanajamii wote wanaoishi jirani na



# Hifadhi ya Arusha yaboresha mazingira ya kujifunzia Ngongongare



Afisa uhifadhi Mwandamizi Mary Mtenga akiwa anatoa elimu ya uhifadhi kwa wanafunzi wa shule ya sekondari Ngongogare

**Na Mwalimu Eliona Milley**

Shule ya Sekondari Ngongongare ni miongoni mwa shule za serikali zilizopo katika vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa Arusha. Shule hiyo ipo katika kijiji cha Ngongongare, kata ya Maji ya Chai wilaya ya Arumeru mkoani Arusha.

Kwa kushirikiana na jamii, Hifadhi ya Taifa Arusha imesaidia shule hiyo kujenga vyumba vya madarasa, kuanzisha vitalu vya miche ya miti, kutoa elimu ya uhifadhi na kuwezesha wanafunzi na walimu wa shule hiyo kutembelea hifadhi bila malipo.

Kutokana na mahusiano mazuri baina ya Hifadhi na kijiji, shule ilipata pia mradi wa ujenzi wa nyumba ya mwalimu na maabara kwa ajili ya wanafunzi kujifunza kwa vitendo.

"Hifadhi imechangia kukuza kiwango cha ufaulu wa wanafunzi wetu hapa shuleni. Tulikuwa na uhaba wa vyumba vya madarasa lakini kutokana na ushirikiano mzuri na Hifadhi wametusaidia ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa, nyumba moja ya mwalimu na jengo la maabara.



Mwl. Eliona Milley wa shule ya sekondari Ngongongare akigawa miti kwa wanafunzi kwa ajili ya kupanda

"Vyumba hivyo vimepunguza msongamano mkubwa wa wanafunzi shuleni na kuwapa mazingira mazuri ya kujifunza na kusaidia kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu" alisema Sophia Warioba ambaye ni Mkuu wa Shule hiyo.

Aidha, Hifadhi kwa kushilikiana na Taasisi ya Jane Goodall kupitia program ya Roots and Shoots ziliwezesha uanzishwaji wa vitalu vya miche ya miti katika Shule ya Sekondari Ngongongare kwa lengo la kurejesha uoto wa asili ambapo miche ya miti zaidi ya 4000 ilipandwa katika maeneo ya shule na mingine kugawiwa kwa wanafunzi, walimu, wananchi na taasisi zilizopo katika Kijiji cha Ngongongare.

Pamoja na mambo mengi yaliyofanyika, Hifadhi ya Arusha ina umuhimu mkubwa sana kwa jamii inayoizunguka pamoja na Taifa zima. Hii inajumuisha kuwa makazi ya wanyamapori, wadudu, ndege na mimea. Pia hifadhi ina misitu ambayo ni mapafu ya kuvuta hewa chafu ya ukaa na inatupatia hewa ya Oksijeni. Aidha, hifadhi hii ni moja ya chanzo kikubwa cha maji katika Bonde la Pangani linalohudumia mikoa mitano ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga na Dodoma

Hifadhi hii ina urithi mkubwa wa sehemu ya mila ya jamii ya wameru kwa ajili ya matambiko hasa pale viongozi wao walipoona majanga ya ukame, magonjwa na vifo yanatokea katika jamii.

Hifadhi pia inatoa ajira kwa watanzania ikiwemo wanaolinda hifadhi, waongoza wageni na jamii inayozunguka hifadhi. Pia inalipatia Taifa fedha za kigeni ambazo zimekuwa zikitumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile vituo vya afya, madarasa, barabara, vifaa vya maabara na utafiti wa kielimu.



# MKOMAZI YAWA MKOMBOZI KWA WAKAZI WA KIJIJI CHA MHEZA



Vyumba vya madarasa vilivyojengwa na TANAPA kwa ushirikiano wa jamii

**Na Tumaini Hozza**

tumaini.hozza@tanzaniaparks.go.tz

Shule ya Sekondari Kwambegu ni shule pekee iliyopo katika kijiji cha Mheza, ambacho ni kati ya vijiji ishirini vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa Mkomazi. Kijiji cha Mheza kipo katika Kata ya Maore, Tarafa ya Ndungu, Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro.

Shule ya Sekondari Kwambegu ilianzishwa mwaka 2017 baada ya shule ya Sekondari Gonja kukumbwa na changamoto ya ongezeko kubwa la wanafunzi kwani ilikuwa shule pekee ya Sekondari katika Kata ya Maore. "Kuanzishwa kwa

shule hii kumesaidia kupunguza adha ya wanafunzi kutembea umbali mrefu kutoka maeneo ya Nadururu, Mheza na maeneo ya kata ya Vuje". Alisema Mhe.Issa Juma Rashidi, Diwani wa kata ya Maore.

Shule ya Sekondari Kwambegu ilianza ikiwa na vyumba vya madarasa viwili na ofisi moja ya walimu, na baadae madarasa zaidi matatu yalijengwa. Mkuu wa shule ya Sekondari Kwambegu Godwin Kitale, alieleza kwamba "Kutokana na ongezeko la wanafunzi, shule ilikumbwa na changamoto ya uchache wa vyumba vya madarasa, jambo lililopelekea Kijiji kuomba Hifadhi ya Taifa Mkomazi kupitia kitengo cha Uhifadhi-Mahusiano Jamii kusaidiwa ujenzi wa madarasa mawili na ofisi moja ya walimu".

"Mradi ulijumuisha ujenzi wa madarasa mawili, ofisi moja ya walimu na uwekaji wa samani yaani meza na viti kwa ajili ya wanafunzi na walimu. Mradi ulitekelezwa kwa ushirikiano kati ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania - TANAPA na wananchi wa Kata ya Maore". Alieleza Kitale.

"Kukamilika kwa mradi huu kumekuwa msaada mkubwa kwa wakazi wa Kijiji cha Mheza na vijiji jirani kwani kwa sehemu kubwa umeweza kutatua changamoto ya uchache wa madarasa katika shule ya Sekondari Kwambegu na kuboresha utoaji wa huduma ya elimu shuleni hapo. Mradi huu unahudumia wakazi wa kijiji cha Mheza na vijiji jirani vya Maore, Kadando, Mpirani, Ntenga na Vuje" Alisisitiza Kitale.

Kamishina Msaidizi wa Uhifadhi, Hifadhi ya Taifa Mkomazi, Emmanuel Moirana alisema kuwa lengo kuu la kutekeleza mradi huu ni kuwafanya wananchi wa vijiji vinavyopakana na Hifadhi kuwa sehemu ya uhifadhi na kuthamini uhifadhi wa maliasili kwani ushiriki wa jamii unahitajika.

"Ni matarajio ya TANAPA kuwa madarasa na ofisi ya walimu yatatunzwa vizuri ili utoaji wa huduma kwa jamii kuwa endelevu. Hivyo basi ni vyema wananchi katika vijiji vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa Mkomazi wakatambua kuwa fedha zinazotolewa na TANAPA katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa jamii ni matunda ya uhifadhi, hivyo kuhifadhi rasilimali za Taifa ni jukumu letu sote". Alisema Kamishna Moirana.

***Uhifadhi endelevu kwa maendeleo ya jamii.***



Kitabu cha Utoaji wa

# ELIMU YA UHIFADHI WA MALIASILI

Kwa Shule za Msingi na Sekondari Tanzania

**Programu ya Hifadhi Zetu, Urithi Wetu**




**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**
**HIFADHI ZA TAIFA TANZANIA**